



# CHUO KIKUU DAR ES SALAAM

## MAFUNZO YA UJASIRIAMALI KWA WAHITIMU WA VYUO VYA ELIMU YA JUU TANZANIA [GRADUATES ENTREPRENEURSHIP PROGRAM (GEP) TRAINING]

### “Badili changamoto kuwa fursa”

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam anawatangazia wahitimu wote wa Vyuo vya Elimu ya Juu Tanzania kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeandaa mafunzo ya ujasiriamali yatakayotolewa katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Unguja, Pemba, Tabora, Mwanza, Mbeya na Ruvuma. Mafunzo haya yataanza mwezi Septemba hadi mwezi Oktoba mwaka 2022.

### LENGO KUULA MAFUNZO

Kuwapatia vijana uelewa, taarifa, maarifa, ujuzi na uwezo wa kuainisha fursa zinazowazunguka na kuweza kuzitumia fursa hizo kuanzisha ajira/biashara kwa ajili yao na wenzao na hivyo kuboresha maisha ya jamii kwa ujumla.

### MALENGO MAHUSUSI

- Kujenga uwezo na tabia ya kuona matatizo na changamoto kama fursa zitokanazo na taaluma zao.
- Kukutana na kujifunza kutoka kwa wajasiriamali wazoefu kutoka kwenye sekta mbalimbali kama vile, kilimo, ufugaji, madini, viwanda na huduma.
- Kutengeneza michanganuo ya mawazo ya kibiashara ambayo itawasaidia kuanzisha biashara na kutafuta mitaji.
- Kuwaunganishavijana wenye mawazo mazuri ya ujasiriamali na watoa huduma za kifedha, teknolojia, uatamizi, nk.

### WALENGWA

Mafunzo haya yanawalenga **vijana** wahitimu wa Vyuo vya Elimu ya Juu kuanzia ngazi ya Diploma na kuendelea wenye nia ya kujiajiri.

### MUDA WA MAFUNZO

Mafunzo haya yatatolewa katika makundi ya watu wasiozidi 50 kwa darasa, kwa muda wa siku nne mfululizo.

### RATIBA YA MAFUNZO

Mahali	Tarehe za Mafunzo	Mwisho wa Kujisajili
Dar es Salaam	27/09- 06/10/2022	23/09/2022
Dodoma	12- 20/10/2022	07/10/2022
Unguja	12 - 20/10/2022	07/10/2022
Pemba	12 - 20/10/2022	07/10/2022
Tabora	12 - 20/10/2022	07/10/2022
Mwanza	12 - 20/10/2022	07/10/2022
Mbeya	12 - 20/10/2022	07/10/2022
Ruvuma	12 - 20/10/2022	07/10/2022

### GHARAMA ZA MAFUNZO

Washiriki hawatalipa ada yeyote ya ushiriki wa mafunzo, ila watajigharamia usafiri na malazi (kama ikilazimu).

### JINSI YA KUSHIRIKI

Jisajili kwa kujaza fomu ya maombi mtandaoni kupitia <https://udsm-gep.ac.tz/> ukiainisha:

- i. Majinayako na nambayasimu.
- ii. Mkoa utakapohudhuria mafunzo.
- iii. Ambatanisha nakala ya cheti cha kuhitimu masomo yako ya elimu ya juu.

Kwa changamoto zozote katika kuwasilisha maombi wasiliana nasi kupitia:

- Barua pepe kwenye anuani: [udiec@udsm.ac.tz](mailto:udiec@udsm.ac.tz)
- WhatsApp no.: +255-734-669-818
- Au +255 745 015 421 kwa msaada zaidi.

### “WAHI KUJIANDIKISHA NAFASI NI CHACHE”

#### Kwa Mawasiliano Zaidi:

Mkurugenzi, Kurugenzi ya Ubunifu na Ujasiriamali,  
Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam  
S.L.P 110099 Dar es Salaam  
Simu: +255-787-805-653; +255-737-828-091